REVIVAL NEWS
From Revival Ministries Australia
P.O. Box 2718 BC TOOWOOMBA Q4350 Australia
Phone: 61-7-46130633; e-mail: rma@revivalministries.org.au
Website: www.revivalministries.org.au

****** NOVEMBA 2020 **** NOVEMBA 2020 **** NOVEMBA 2020 ******

DHAMIRI

Na Nicholas Jackson

Mungu alituumba na dhamiri. Ni uwezo ambao unatuwezesha kuyashika mapenzi ya Mungu, kama kile ambavyo umewekwa kutawala maisha yetu [kutoka kwa the best of Vines Dictionary in the Strong's Concordance, Greek#4893]. Ni uwezo wenye nguvu ambao hukaa ndani ya roho yetu na kutupa uadilifu wa kidhamira, uwezo wa kujua mema na baya. Katika lugha ya Kigiriki ni neno 'suneidesis' na hasa linamaanisha kujua, kuwa na kujijua mwenyewe. Dhamiri ni sehemu katika roho yetu ambapo tunajua vitu, si kwa sababu tumefundishwa, bali ni kujua kwa kiasili ndani yetu kwa sababu ya kuumbwa kwa mfano na sura ya Mungu. Mungu kila mara alikusudia tutawaliwe katika maisha yetu na dhamiri ambayo alituumba nayo.

Kuhukumika na dhamiri yetu

Waandishi na Mafarisayo walimleta mwanamke ambaye alishikwa kwa uzinzi kwa Yesu kwa lengo la kumshika na kumshtaki kuhusu sharia ya Musa (Yoh.8:1-6).Yesu alikuwa na neno la hekima kupitia kwa Roho, "Yeye asiye na dhambi miongoni mwenu awe wa kwanza kumtupia jiwe" (Yoh.8:7).Baada ya kuandika kwenye ardhi na kusema neno hili, inasema kuhusu Waandishi na Mafarisayo, "Nao waliposikia,wakashitakiwa na dhamiri zao wakatoka mmoja mmoja, wakianzia tangu wazee hata na wa mwisho wao"mst.9.

Walihukumiwa na dhamiri yao. Neno kuhukumiwa lina maana: kushauriwa, kupingwa, kuletwa kwenye nuru, kuwekwa wazi, kukaripiwa, kushtumiwa, kuadhibiwa [Strong's Concordance Greek# 1651, pia Thayer's]. Nina hakika sote tumepitia hii saa nyingine. Ni la kushangaza kwa nguvu kuanuliwa, kushauriwa, kushtumiwa na kukaripiwa na dhamiri yetu. Hii ni wakati tunapotambua kwamba kile ambacho tumefanya ni kibaya sana na kisha tunahisi aibu ikianza kutufunika kama blanketi. Inaweza kuwa na nguvu sana hata ikabadilisha matendo yetu kabisa!

Kujionyesha kwa dhamiri ya kila mtu

Dhamiri ina nguvu! Hawa watu walikuwa wanamtumia mwanamke kama kishawishi kujaribu kumshtaki Yesu ;mbinu fisadi na ovu kabisa. Walikuwa tayari kumtoa huyu mama dhabihu, kufanya auawe na kumwaibisha kwa sababu ya nia yao ovu! Hii ilibadilika kiajabu kwa neno moja la hekima kutoka kwa Mungu. Neno lilifunua ukweli. Dhamiri ya hao wanaume iliwahukumu na tabia yao ikabadilika mara. O, laiti tunene kama Yesu na tuone athari yake kwa walewanaotuzunguka pia! Laiti tunene kwa njia ambayo inahukumu dhamiri za wale wanaotusikiliza! Mtume Paulo alisema, "lakini kwa kuidhihirisha iliyo kweli twajionyesha kuwa na haki, dhamiri za watu zikitushuhudia mbele za Mungu". Kwa kusema ukweli wa Neno tunajionyesha kukubaliwa kwa dhamiri ya mwanadamu, kuleta dhamiri ya huyo mtu kwenye uwepo wa Mungu ambapo fikira na matendo yao yanafunuliwa katika nuru Yake!

Kuwa na dhamiri isiyo na hatia

Paulo alipokuwa hukumuni mbele ya Gavana Felix alisema, " Nina tumaini kwa Mungu, ambalo hata hao nao wanalitazamia, ya kwamba kutakuwa na ufufuo wa wafu, wenye haki na wasio haki pia. Nami ninajizoeza katika neno hili niwe na dhamiri isiyo na hatia mbele za Mungu na mbele ya watu siku zote" Matendo 24:15-16. Tumaini tulilo nalo katika ufufuo na hukumu unaokuja linafaa kutuamsha kuishi bila hatia na kushtakiwa katika dhamiri yetu.

La kusisimua ni kwamba Paulo anasema hatia hizi zinaweza kuwa dhidi ya Mungu na binadamu. Ni muhimu kwamba tusishikilie mashtaka ambayo pengine tunabeba kisiri dhidi ya Mungu, kumshtaki kwa mabaya katika dhamiri yetu. Wengi wetu tumekuwa na vitu vimefanyika katika maisha yetu ambavyo vimeleta uchungu na maumivu ya kiroho na pengine tumemlaumu Mungu na tunabeba hatia dhidi yake. Pengine tumewaombea watu na hakuna kilichofanyika,na tukasikitishwa na Mungu na kuanza kuwa na malalamishi ndani ya moyo yetu dhidi yake. Ni muhimu kushughulikia hii na kuachilia hatia zote. Stefano, mfiadini, hakubeba uchungu yoyote naye kwenda kwa utukufu. Maneno yake ya mwisho yaliyoandikwa yalikuwa, "Bwana usiwahesabie dhambi hii" Matendo 7:60.

Fundisho ni muhimu kwa dhamiri yetu

Mtume Paulo alimwambia Timotheo, "uwakataze wengine wasifundishe elimu nyingine" 1 Tim.1:3. Kisha anasema, "Walakini mwisho wa agizo hilo ni upendo utokao katika moyo safi na dhamiri njema, na imani isiyo na unafiki" 1 Tim.1:5. Kusudi la hii amri kutofundisha lolote lisilokuwa "fundisho la mitume" (Matendo 2:42), ni kutoa upendo kutoka kwa dhamiri safi. Fundisho la kweli likiishi ndani yetu huleta matokeo ya maisha ya upendo wa kweli kutoka kwa dhamiri iliyo wazi kwa sababu ya nia wa moyo safi.

Usichome dhamiri yako

Kinyume pia ni kweli kwamba "tukisikiliza roho za udanganyifu na mafundisho ya pepo" tunaishia "kusema uongo kwa unafiki, tukichomwa moto dhamiri zetu wenyewe"1 Tim.4:1-2. Chungana na mafundisho ya "kanisa" ambayo yanafunga watu kidhehebu, kidini! Kwa bahati mbaya, wengine wanaweza kushikwa kufundisha na kuhubiri vitu wanavyojua katika dhamiri yao si kweli! Ukiendelea kufanya hivi, unaweza kuchoma dhamiri yako kwa pasi moto. Hii inamaanisha kwamba itapunguza na kupunguza kuwa na hisia kwa ukweli. Una haki na hata inakupasa kusikiliza dhamiri yako na kukosa kuhubiri na kufundisha kinyume chake. Unavyozidi kusikia Neno la kweli la Mungu, ndivyo dhamiri yako inavyoendelea kujifungua kwa ukweli na ndivyo dhamiri yako itakavyokuchoma kama kitu iko dhidi ya kweli. Sikiliza dhamiri yako.

KUSAFISHA DHAMIRI ZETU

Kuwa na dhamiri kamilifu

Chini ya Agano la Kale ibada za Hema zilikuwa "ndiyo mfano wa wakati huu uliopo sasa; wakati huo sadaka na dhabihu zinatolewa, zisizoweza kwa jinsi ya dhambi kumkamilisha mtu aabuduye kwa mambo ya kuhusu dhamiri" Waebrania9:9. Dhabihu na bada zilizofanywa chini ya Agano la Kale hazingetufanya kamilifu kwa dhamiri. Mungu anataka tuwe na dhamiri kamilifu. Hii inamaanisha kuwa na dhamiri iliyokomaa, timilifu, nzima na kamilifu. Dhabihu za wanyama chini ya Agano la Kale hazingeifanya kwa sababu "ziliamriwa hata wakati wa matengenezo mapya" Waebrania 9:10. Sasa tuko katika wakati wa matengenezo mapya! Kile kilichokuwa mfano sasa kinachukua umbo. Yesu amekuwa dhabihu kamili na anaweza, kupitia kwa dhabihu hiyo,kukamilisha dhamiri zetu.Inawezekana kuishi na dhamiri kamilifu, isiyochafuka mbele za Mungu!

Hakuna dhamiri ya kuwa na dhambi tena

Katika Waebrania 10:1-2 sisitizo tena ni kwa kutoweza kwa dhabihu za Agano la Kale kutufanya wakamilifu, kwa kuwa sheria "ni kivuli cha mema yatakayokuwa, wala si sura yenyewe" (mst.1) na kwa hivyo haiwezi kutukamilisha. Kama ingetufanya wakamilifu basi "hazingekoma kutolewa; kwa maana waabuduo, wakiisha kusafishwa mara moja ,wasingejiona tena kuwa na dhambi? mst.2.Hii inastaajabisha! Neno kuwa na dhamiri ni sawa na neno la Kigiriki [Strong's Greek#4893-'suneidesis'] linatafsiriwa kama dhamiri mahali pengine. Mpango wa Mungu kila mara umekuwa ni hatimaye kutoa ndani yetu hasa kuwa na dhamiri ya dhambi. Dhabihu ya Yesu ndiyo "sura kamili" ya vivuli ambavyo vilikuwa dhabihu za wanyama chini ya torati.

Dhabihu ya Yesu huondoa kujua dhambi katika maisha yetu. Hatuwi tena na dhamiri ya dhambi. Tunakuwa na kujua sana na sana nguvu za dhabihu ya Yesu na haki ambayo tumewekewa kwa imani ndani yake! Sasa tunakuwa na dhamiri ya "Kristo ndani yetu; tumaini la utukufu" Wakolosai 1:27. Hatuna tena dhamiri ya dhambi ambazo tumetenda kwa sababu dhabihu ya Yesu imezishugulikia zote na sasa "Yesu Kristo yumo ndani yenu" 2 Kor.13:5. Hatuhitaji kuishi tukikumbushwa juu ya dhambi zetu tena. "Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha kutokana na udhalimu wote"1 Yoh.1:9. Tunaishi katika dhamiri ya kusamehewa, kukombolewa, ufanywa haki, kufanywa wana, na kutukuzwa!(Waefeso 1:5-7,Warumi 8:30).Huu ni uhuru wa jinsi gani! Tuna "mwombezi kwa Baba" 1:Yoh.2:1.Dhabihu yake inatosha! Sasa tuna dhamiri ya Yesu na yale ambayo amekamilisha!

Kusafishwa kutoka kwa matendo mafu

Dhabihu za Agano la Kale ziliweza tu "kutakasa hata kuusafisha mwili" Waebrania 9:13b. Zingesafisha tu kisherehe, kidini na ki-nje. Haingeshughulika na dhamiri. Lakini "basi zaidi damu yake Kristo, ambaye kwamba kwa Roho wa milele alijitoa nafsi yake kwa Mungu kuwa sadaka isiyo na mawaa, itawasafisha dhamiri zenu na matendo mafu, mpate kumwabudu Mungu aliye hai? Waebrania 9:14. Kwa kuwa Yesu alikuwa Mungu katika mwili, aliweza kujitoa "Roho wa milele". Damu ya Yesu hakika inaweza kufanya kazi katika sehemu zisisoonekana ndani yetu, katika roho zetu, na kuathiri dhamiri yetu. Damu ya Yesu hufanya kazi kiroho na kushughulika na shida za dhamiri isiyo safi.

Kumtumikia Mungu aliye hai

Damu ya Yesu inaweza kusafisha dhamiri zetu kutoka kwa matendo mafu kumtumikia Mungu (Waebrania 9:14b). Wakristo wengi hufanya makosa ya kujaribu kumtumikia Mungu ili kusafisha dhamiri yao. "Nikimfanyia tu Mungu hivi vitu vyote basi dhamiri yangu itakuwa safi", "Nikienda kanisani na kulipa zaka zangu basi nitakuwa sawa na Mungu kwa dhamiri yangu". Hii ni fikira mbaya. Hayo ni matendo mafu. Hakuna kiwango cha kujaribu kumuishia Mungu kitaweza kusafisha dhamiri. Ni damu ya Kristo tu ambayo inaweza kusafisha dhamiri zetu. Sisi hutembea kwa imani!

Tunapoweka imani yetu kikamilifu katika nguvu na uwezo wa damu ya Kristo kusafisha dhamiri yetu tutapata mwachilio ya uhuru kubwa! Tutakuwa na dhamiri safi, wazi na nzuri na kisha tutaweza Kumtumikia Mungu aliye hai! Tunasafishwa kutoka kujaribu kufanya matendo ya kidini kusafisha dhamiri zetu. Tunapata dhamiri zetu kusafishwa na damu ya Yesu ili tuweze kumtumikia Mungu kama tumeondolewa hatia na lawama. Mtume Paulo, hata baada ya historia yake kali dhidi ya waumini katika Yesu, aliweza kusema, "Ninamshukru Mungu wangu, nimwabuduye kwa dhamiri safi…2 Tim.2:3. Laiti sisi pia tujifunze kutumika kwa na kutoka kwa dhamiri safi, iliyosafishwa! Kisha utakuwa na ujasiri na kushuhudia kazi za Mungu za ajabu katika maisha yako!

Kunyunyizwa kutokana na dhamiri ovu

Kwa sababu ya kuwa na “ujasiri wa kupaingia patakatifu kwa damu ya Yesu, kwa njia ile iliyo mpya, iliyo hai” (Waebrania 10:19-20a) tunaweza “kukaribia wenye moyo wa kweli, kwa utimilifu wa imani, hali tumenyunyiziwa mioyo tuache dhamiri mbaya” (Waebrania 10”22). Kunyunyiziwa kulikorejelewa hapa ni “kunyunyizwa kwa damu ya Kristo” (1 Pet.1:2) na pia kumerejelewa kama “Damu ya kunyunyizwa inenayo mema kuliko ile ya Habili” (Waebrani 12:24). Mioyo yetu imenyunyizwa na damu ya Yesu na “tumenyunyizwa kutokana na dhamiri mbaya”.

Neno ovu ni la kusisimua. Ni neno la Kigiriki peneros na linamaanisha: lakuumiza, ovu katika athari au ushawishi kinyume na kuwa ovu kimsingi. Linamaanisha kuwa na janga, kuwa na ugonjwa,wa kulaumika, wenye hila,kali, wa kukasirisha, uliojaa ugumu, uliofinyika, uliodhulumiwa, unaleta uchungu na shida [Strong’s ConcordanceGreek #4190 & Thayer’s].

Mungu hataki uishi na dhamiri ambayo inakudhulumu, kuwa kali kwako, kukuletea uchungu au shida, kukukasirisha au kuwa nahila mbaya na kukuchezea! Anataka uishi huru kutokana na majuto, na athari ya mateso ya dhambi za kale na maamuzi mabaya ambayo tumefanya! Wacha damu ya Yesu inyunyize moyo wako kutokana na dhamiri hii hatari ambayo haikuachilii. Ni wakati wa kuwa huru kutokana dhamiri mbaya na kujifundisha kutembea katika dhamiri safi iliyosafishwa! Wakati mwingine tunafikiri ni shetani anatudhulumu lakini inaweza kuwa hasa ni dhamiri yetu wenyewe. Kama ni shetani unaweza kumtupilia mbali. Lakini huwezi kutupa dhamiri yako! Unahitaji kunyunyizwa na damu ya Yesu! Ndiyo suluhisho pekee!

Jibu la dhamiri nzuri

Mtume Petro anaeleza kwamba wokovu wa Nuhu na jamii yake ndani ya safina wakati wa gharika ina “mfano-kielezo [kifananishi au utimizo] ambacho sasa hutuokoa-ubatizo (sio kutoa uchafu wa mwili, bali jibu la dhamiri nzuri mbele ya Mungu), kupitia kwa ufufuo wa Yesu Kristo”1 Pet.3:21.Ubatizo hautuokoi kwa kutoa uchafu wa mwili. Ni damu ya Kristo ndiyo husafisha dhamiri yetu na kutunyunyiza kutokana na dhamiri mbaya! Lakini jibu la dhamiri nzuri, dhamiri iliyosafishwa, ni kubatizwa kwenye nguvu za ufufuo wa Yesu ili uweze “kuenenda katika upya wa uzima” Warumi 6:4b.Kwa kuamini katika kifo na kufufuka, damu ya Yesu hufanya kazi kusafisha dhamiri zetu kutoka kwa dhambi, matendo mafu na yanayo kutudhulumu.Matokeo na jibu la dhamiri hiyo ni kuingia maisha ya ufufuo kupitia ubatizo ndani ya Kristo na kuishi dhamiri ya kujua dhambi tena!

Kuishi katika dhamiri nzuri

Paulo aliponena kwa Waebrania alipokamatwa Yerusalemu alisema, “Ndugu zangu, mimi kwa dhamiri safi kabisa nimeishi mbele za Mungu hata hivi leo” Matendo 23:1.Tunapaswa kuweka dhamiri safi mbele za Mungu. Je, hii inamaanisha hatutendi dhambi? La hasha. Lakini inamaanisha tunawajibika kwa dhambi zetu dhamiri zetu zinapotuhamasisha kuhusu dhambi na tunatubu, kukiri dhambi zetu na kuamini katika damu kutusafisha na kutusamehe. Dhamiri nzuri hutufanya kuwa na ujasiri katika imani na kuweza kuenenda kwa unyoofu na kwa umairi katika kujua kwamba Mungu yu nasi, “Nanyi muwe na dhamiri njema, ili katika neno lile mnalosingiziwa, watahayarishwe wale wautukanao mwenendo wenu mwema katika Kristo” 1 Pet.3:16 .Sikiliza dhamiri yako. Kumbuka kwamba fundisho la kweli linafaa kuleta upendo…kutokana na dhamiri njema (1 Tim.1:5) na kwamba tunafaa “kuwa na umairi kwamba tuna dhamiri njema, tukitaka kuwa na mwenendo mwema katika mambo yote” Waebrania 13:18.

Na hatimaye, ndugu wapendwa,

mkubali Mungu kukamilisha, kusafisha

na kunyunyiza moyo wako

kutoka kwa dhamiri mbaya

ili uwezekuwa huru

kumtumikia mungu aliye hai!